

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI**

**06 JUNI, 2024**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI TAREHE 06 JUNI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

542. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE  
(TABORA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaipatia Hospitali ya Wilaya ya Uyui gari la Wagonjwa.

**543. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali inaridhishwa na ujenzi unaoendelea wa Ofisi ya Halmashauri ya Masasi DC na Hospitali yake na juhudi gani zinafanyika kuinusuru.

**544. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR (NYANG'HWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Vituo vya Afya Kharumwa na Nyang'hwale vitapatiwa X - Ray.

**545. MHESHIMIWA JANEJELLY JAMES NTATE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaajiri Wataalam wa kuendesha mikopo ya Halmashauri ya asilimia 10 badala ya kufanywa na Maafisa Maendeleo ya Jamii.

**546. MHESHIMIWA JONAS VAN ZEELAND  
(MVOMERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Doma Kijiji cha Boma Wilayani Mvomero.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**547. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO  
(MIKUMI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina Mpango gani wa kutunza mazingira ya Bwawa la Zombo Kilosa ili litumike kwa Shughuli za ufugaji wa Samaki na Kilimo.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**548. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI  
MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha utalii Kihesa Kilolo chini ya mradi wa *Regrow*.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**549. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, kuna mpango gani kuvipatia mawasiliano ya simu Vijiji 13 na Kata za Mughunga, Ngimu, Makuro, Mudida, Ughandi, Msisi, Msange na Mgori.

**IV. HOJA BINAFSI ZA WABUNGE:**

**MHE. PRISCUS JACOB TARIMO**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kujadili Hoja kuhusu Halmashauri za Miji na Wilaya Kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutatua tatizo la Upungufu wa Magari ya Zimamoto pamoja na Vifaa vinavyotumika kuzima Moto na Uokoaji.

**DODOMA  
06 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**